WARSHA YA VIONGOZI WA MILA JUU YA MAFUNZO YA UWAKILISHI, USHIRIKISHWAJI NA UONGOZI KWA AJILI YA USIMAMIZI NA MATUMIZI ENDELEVU YA MALIASILI, ILIYOFANYIKA KIJIJI CHA SINYA WILAYA YA LONGIDO KUANZIA TARAHE 30-31/05/2007.

Utangulizi:

Wilaya ya Longido ni makazi ya jamii ya Kimaasai ambao ni asilimia zaidi 90% ya wakazi wa wilaya hiyo, kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002. Wilaya hii hupata mvua kiasi kidogo kwa mwaka, na hivyo shughuli za kiuchumi zinazotegemewa na wenyeji ni ufugaji, biashara na utalii. Ila kwa upande wa vijiji vinavyozunguka mlima wa Kilimanjaro kama Elerai na Irmolok wananchi hutegemea kilimo na ufugaji. Maeneo mengine katika ukanda wa chini jamii hutegemea ufugaji tu.

Ufugaji ndio uti wa mgongo wa jamii ya wamaasai waishio wilaya ya Longido, ni asilimia kidogo tu ya wenyeji hujishughulika na kilimo cha jembe la mkono. Kilimo imeonekana kuwa ni muhimu kwa familia nyingi hasa wakati wa kiangazi, ng'ombe wakiwa dhaifu. Kutawanyisha njia za kiuchumi wilayani Longido ni muhimu ili kuondoa familia nyingi katika hali duni ya maisha hasa uhakika wa chakula. Baadhi ya vijiji wilayani Longido wameanzisha miradi ya utalii kushirikiana na makampuni ya kitalii. Miradi hii imewasaidia wanavijiji kujiletea maendeleo ya jumla, ila bado ni kwa kiwango kidogo tu.

Mifumo ya maisha kwa jamii hii hutegemea hali halisi ya mazingira na maliasili zilizopo. Jamii ya wafugaji wa kimaasai wilayani Longido wamejiwekea utaratibu wa kimila unaowawezesha kila mmoja kupata na kutumia raslimali kama vile maji, malisho, chumvi ya asili, bila kujali mipaka ya kiutawala, umbali au tofauti za koo. Mfumo huu wa maisha umeweza kujenga mfumo dhabiti uliosaidia maisha endelevu ya maliasili na maisha ya watu. Taratibu hizi za maisha zinazosimamiwa na mfumo wa utawala wa mila umewawezesha wafugaji kuishi na kuendesha maisha yao kwa amani, upendo na zaidi ya yote kuwezesha maliasili kuendelea kuwepo kwa karne nyingi zilizopita na zijazo.

Wilaya ya Longido ni chimbuko la maliasili hasa wanyamapori wanaotegemewa na jamii kwa nyanja mbalimbali, kama vile utalii, ufugaji na mila. Utajiri wa maliasili ndani ya wilaya ya Longido

umewavutia wengi, hasa makampuni binafsi kuwekeza ndani ya wilaya. Uwekezaji huu ni pamoja na uwindaji wa kitalii, utalii wa kupiga picha na utengaji wa maeneo ya uhifadhi wa wanyama pori ya jamii, (WMAs). [1]Pamoja na uwekezaji huu wa kitalii katika vijiji vya wilaya ya Longido, kumeonekana upungufu mkubwa katika suala zima la uratibu na maamuzi shirikishi toka kwa wananchi. Ushawishi wa uwekezaji umetoka nje na unahitaji utaratibu bayana uliowazi na shirikishi ili kuleta uwiano sawia wa usimamizi na utumiaji endelevu wa maliasili bila kuadhiri maisha ya watu, maliasili na kuepuka migogoro inayoweza kujitekeza.

Utajiri wa maliasili na kutokuwepo wa utaratibu na usimamizi wa maliasili katika wilaya hii, umelete ushindani mkubwa uliyosabisha mgongano ya tawala mbalimbali ndani ya wilaya. Ushindani huo wa matumizi na usimamizi ya maliasili unatokana na mabadiliko katika ngazi mbalimbali ya kiutawala kiuchumi, kisiasa na kijamii, ambapo watu wa wilaya ya Longido wameshuhudia kutetereka kwa mifumo ya usimamizi wa utawala wa jadi uliyosimamia haki na usawa wa matumizi ya mali asili. Utaratibu na utawala wa mila unazidi kutetereka, kukosa nguvu na ushikamano, na hatimaye kutokea migongano baina ya mfumo rasmi na isiyo rasmi, (informal and formal system) wawekezaji na jamii, serikali na vijiji, wawekezaji na wawekezaji hatimaye kusababisha kutokuwepo na uhakika wa kutumia fursa ya uwekezaji ndani ya wilaya na pia kuatarisha usimamizi mzima wa ardhi na maliasili.

> *Mifano halisi ya uwekezaji na matatizo yake ni kama mikataba ya utalii katika vijiji, kama Sinya, Uwindaji na utalii wa picha, matumizi ya mipango ya ardhi na utali na migogano ya kampuni za uwindaji na kampuni za utalii wa picha.*

Mifumo ya jadi yalishikilia uwepo wa maliasili na hatimaye maisha ya watu. Kutokana na mabadiliko mbalimbali katika sera na sheria katika Nchi na Kimataifa kumekuwepo na taratibu zingine zinazosimamia maliasili hizi na hatimaye maisha ya watu. Sera na sheria hizi zimeweka taratibu zingine zinazo zingatia uzalishaji wa wa faida, matumizi na usimamizi wa kisasa na unufaikaji wa rasilimali, kubadilisha mifumo ya usimamizi na mamlaka ya kiutawala.

Mwingilio wa sera, sheria na taratibu za mila katika ngazi za vijiji zimesababisha migongano aa matumizi, usimamizi na unufaikaji wa maliasili na hatimaye kuleta hali iliodhorotesha maisha ya wafugaji na kuachwa bila maamuzi dhabiti ya kulinda na kutumia maliasili zao kwa njia ipasavyo. Mgongano wa Sera na sheria ya ardhi na wanyamapori imesababisha wasiwasi ambao umewafanya wananchi wa wilaya ya Longido kubakia katika hali ya kutojua ni jinsi gani wanaweza kutumia ardhi na wanyama pori kuondoa umaskini kwa jamii na familia.

[1] Wildlife Management Areas-A Government proposed project for sustainable management of wildlife outside PA and a wildlife project to benefits local people in the village land.

Vijana wengi wameishia kuwa walinzi katika maeneo mbalimbali ndani na nje ya wilaya ya Longido. Hii ni kutokana na hali halisi ya ugumu wa maisha na kukosekana kwa taratibu za kutumia maliasili kama wanyamapori kuleta ajira na kuondoa umaskini. Ulinzi ikiwa kama ni kimbilio kwa vijana wengi imedhorotesha na kuangamiza maisha ya vijina wengi wa kifugaji. Vijana wengi hawana elimu ya kujua kusoma na kuandika, hivyo kazi wanaoweza kupata ni ulinzi tu.Wanawake nao baada ya kuongezeka kwa umaskini katika familia, hasa kukosekana kwa maziwa ya kutosha kwa watoto, wameanza biashara mbalimbali kama uuzaji wa kuni, pombe na uuzaji wa bidhaa za utamaduni kwa watalii bila mafanikio ya kujikomboa. *Je maisha ya vizazi vijavyo ya jamii hii wa wafugaji, kiuchumi na kiutamaduni itakuwaje?*

Ili kuweza kutafakari maisha ya mbele (future) ya jamii na maliasili Shirika la TNRF, CRT, SCF na kwa ushirikiano na taasisi zingine na baadhi ya viongozi wawakilishi wa jamii, wameona haja ya kuelimisha jamii kupitia, vyombo vya serikali kama serikali za vijiji, mabaraza ya mila na mikutano mikuu juu ya hali halisi ya maisha ya sasa na baadaye na maliasili hasa kuhusisha na sera na sheria zilizopo. Mabaraza ya mila imeonekana kuwa ndicho kitovu cha mhimili ya jamii ya wafugaji kama watapewa nafasi ya kutumia mamlaka waliopewa na jamii kuleta maendeleo endelevu. Hii ni kutokana na mamlaka na uongozi uliopo sasa kutokuwa shirikishi kama ipasavyo na pia kutumia siasa mbaya kufikia maamuzi ya kimsing. Katika kubuni na kutetea uwelekeo wa jamii kisera na kisheria Mabaraza ya mila yanauhalali wa kuwakilishi jamii bila kuwawishiwa na mifumo ya kiutawala wa aina yeyote. Mabaraza ya mila ni kuingo kikubwa sana ya utetezi na uhamasishaji wa maendeleo na kuleta haki ya uwiano wa manufaa yatokayonayo na maliasili katika ngazi ya mbalimbali. Uwiano huo hutegeameana na jinsi gani sera na sheria zilizopo zinapotafisiriwa na kutekelezwa na wananchi katika kuleta maendeleo.

Hivyo basi kumeonekana kuna haja ya kuweka mikakati mahususi ya kifikra za kiuzalendo wa kuhakikisha kuwa kunakuwepo na maisha endelevu ya jamii na maliasili zilizopo na kuleta maendeleo endelevu kwa jamii ya wilaya ya Longido kwa kupitia jitihada za jamii.

Malengo ya Warsha:

- Kuwaleta pamoja jamii ya wafugaji kupitia uwakilishi wa mabaraza ya mila kutafakari mfumo wa maisha ya wafugaji, usimamizi na matumizi endelevu ya ardhi na maliasili kwa sasa na baadaye.
- Kufahamu na kubainisha uhusiano uliopo baina ya mfumo wa kifugaji, sera, kanuni na sheria zinazosimamia maliasilia kama ardhi na wanyamapori.
- Kujenga mikakati ya pamoja wa kukabiliana na misukumo mbalimbali ya kuichumi, kisiasa na kijamii, ili kuweza kunusura jamii ya wafugaji katika wimbi la umaskini.

Mada zilizofundishwa na kujadiliwa:-

Mada ya Kwanza: **Ufunguzi na utangulizi.**

Baada ya utangulizi mwezeshaji alimkaribisha Mkuu wa Wilaya ya Longido Bwana Milia ili aweze kufungua warsha hiyo. DC huyo wa Longido, aliwaeleza wanawarsha kuwa, kihistoria wafugaji ni watu wenye utamaduni unawajali wanyama pori na maliasili nyingine. Aliendeleza kuwa mila na desturi za jamii ya wafugaji imeendelea kuwa changamoto katika kuendeleza maliasili hasa wanyamapori, hivyo ni jukumu la taasisi za maendeleo hasa ya uhifadhi kutambua hili. Aliendelea kusema kuwa baada ya mabadiliko katika mifumo ya maisha kumeonekana haja ya kutafakari mifumo ambao itawawezesha jamii ya wafugaji kunufaika na maliasili inayowazunguka, kama vile wanyamapori, misitu n.k ili kutoa motisha kwa jamii katika kuendeleza uhifadhi huo. Baada ya Mkuu huyo kueleza kwa kirefu umuhimu wa kuwatunza na kufaika na maliasili, aliwaasa wanavijiji waweze kuwa macho hasa katika kuweka mikataba ya uwezekezaji kwani mikataba hiyo inaweza kufunga fursa ambazo zingiweza kutumika kuondoa umaskini kwa wanavijiji.

Mada ya Pili: **Matarajio na Hofu:**

Matarajio na hofu, yalijadiliwa ili kupata hali halisi ya mitazamo na mategemea baada ya warsha na kujenga mkakati ya pamoja. Washiriki walibainisha kuwa ufugaji ni nguzo dhabiti ya kuendeleza mazingira na maisha ya watu. Pia walijadajadili kuwa kuna hasa ya kuweka bayana mambo makuu yafuatayo: - Ufugaji na maliasili zisitengwe, uongozi wa haki ulioshirikishi ndiyo dira ya maisha, mabadiliko kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni yatokane na watu wenyewe na siyo ya kudhaniwa.

Matarajio >'*Osiligi*'
Hofu >'*Olmakurete*'

Mada ya Tatu: **Ardhi na Maliasili na maisha ya wafugaji**

Mada hii ilianza kwa ufafanuzi juu ya mazingira/Ardhi na maliasili kwa kujua nini maana ya mazingira, ardhi na maliasili, kuoanisha mfumo wa ufugaji na mazingira kwa ujumla. Wawezeshaji waliuliza nini maana ya mazingira! Tafsiri nyingi ilitotolewa kuhusu mazingira, ila ilikuwa ni vigumu kupata neno kamili la mazingira hasa kwa mfumo wa wafugaji. kwani walieleza mazingira katika mitazamo mingi kama:-

- Mazingira ni maisha ya mtu na vyote anavyotegemea mtu kuishi.
- Mazingira ni kitovu cha maisha, na ndicho kinachotuwezesha mtu kuishi, kustarehe na kunufaika na hatimaye kuwa na maisha endelevu kwa binadamu na mifugo.

Washiriki walibainisha kuwa mfumo wa ufugaji ni nguzo dhabiti ya kuendeleza mazingira na ndiyo sababu sehemu wanamoishi wafugaji zimafanywa maeneo maalum kwa ajili ya uhifadhi. Mfano Ngorongoro, serengeti, Lake Natron, Loliondo, Mkomazi, Masai mara, Tarangire, manyara n.k.

Baada ya kuojadiliana kwa muda mrefu mambo mawili makuu yalijitokeza na kubeba mada nzima ya uhusiano wa ufugaji, mila na desturi za wamaasai na uhifadhi wa malilasili ambazo ni

- Mazingira endelevu,
- Manufaa ya maliasili kwa wafugaji

Kwa misingi hiyo, washiriki waliona kuwa kuna haja ya kuweka mikakati ya matumizi endelevu ya ardhi na malisaili kwa kuzingatia mfumo wa ufugaji, ongezeko la watu, mabadiliko ya kiuchumi na kijamii na sera na sheria zinasimamia malisaili hizo. Ilionekana kuwa ongezeko la watu, mifumo ya kiuchumi na mabadiliko katika utamaduni umesababisha kuwepo kwa chimbuko la uharibifu wa mazingira, migogoro ya matumizi na usimamizi wa maliasili, kutungwa kwa sera na sheria inayozingatia faida na uhifadhi wa maliasili pasipo kujali maisha ya watu na utamaduni.

Kutokana na mabadiliko katika mfumo wa uchumi wa fedha, unaozingatia faida bila kujali mazingira na mfumo unaoendeleza mazingira (Ufugaji wa asili), jamii imejikuta haina maeneo ya kutosha kwa ufugaji, akiba ya baadaye na hata haki ya kumiliki ardhi na maliasili hiyo kwa mujibu wa sheria zilizopo. Mfano sheria ya ardhi ya vijiji N0, 5 ya 1999, inatoa nafasi ya umiliki ya ardhi ya kimila, lakini sheria zingine zimepewa kipaumbele ya kutumia ardhi hiyo pasipo makuabaliano ya msingi na jamii inayioshi katika ardhi hiyo, kama sheria ya maeneo tengefu (GCA) [2]inapingana sheria ardhi ya vijiji, na hatiamye kusababisha uporaji wa ardhi kwa jamii ya wafugaji.
Mifano halisi ni kitalu cha uwindaji ya wanayamapori Loliondo, Mondoli, Simanjiro na Longido.
Maazimio katika eneo hili ni:-

- Serikali itambuwe maeneo ya wafugaji na ipewe kipaumbele ili isinyakuliwe kupitia dhana ya uhifahi ya maliasili kama wanyamapori.
- Kuondoa mgongano wa kisheria baina ya sheria ya ardhi na ya wanyamapori inayosimamia mapori tengefu (GCAs)

Mada ya Nne **Uwekezaji na Maendeleo ya wafugaji.**

Kutokana na sera za kiuchumi duniani kumekuwepo na makubalinao baina ya mataifa yalioendelea na yanayoendelea kama Tanzania, kuwa nguzo ya kuondoa umskini ni kuboresha ushirikiano wa kimatifa katika biashara. Sera za uchumi wa dunia ni mahusiano baina ya Nchi zilizondelea na zinazoendelea katika uimarishaji uchumi wa dunia. Hivyo neno uwekezaji ni njia mojawapo ya

[2] Game control Areas is supported by wildlife legislation which allows a multiple land use in village land, but it fevers the interest of wildlife hunting.

kuwaruhusu watu toka nje kuja kutumia maliasili kama ardhi, wanyamapori, kutumia na kuwekeza viwanda katika nchi nyingine ili kuboresha biashara.

Baada ya mijadala mirefu katika agenda hii, washiriki waliuza maswali mengi, na baadhi ya maswali hayo ni:-

- Uhusiano wa biashara unalengo la kumkomboa nani baina ya Nchi zilizoendelea na Nchi zinazoendelea?
- Uwekezaji huo wa kiuchumi umeleta manufaa gani hasa kwetu Tanzania?
- Je wafugaji wananufaikaje na uwekezaji huo?

Uwekezaji ulijadliwa kwa mapana kwa kutazama njia mbalimbali hasa katika ngazi ya Taifa na kijiji. Baada ya kuona kuwa uwekezaji katika ngazi ya kijiji ni kama uwidaji wa wanyamapori, utalii wa picha, kilimo cha kisasa, misitu na madini. Washiriki walitafakari uwekezaji unaoendelea katika wilaya ya Longido kama uwindaji wa wanyamapori, WMAs, Utalii wa picha, kilimo na maeneo binafsi ya wanyampori kama Entarakuai. Walisema kuwa pamoja na uwekezaji huu wenye nia ya kuboresha uchumi, wafugaji wanajikuta wakinyanyasika na kunyimwa haki yao katika maamuzi. Walisema kuwa maamuzi yanayotolewa hasa katika kuruhusu uwekezaji hufanyika nje bila kuhusisha watu na matokeo yake ni migongano makubwa na hatimaye manufaa yatokanayo na uwekeza huo kwenda mikononi mwa wachache. Waliendelea pia kusema kuwa baadhi ya wawekezaji wameleta misaada isiyoleta madadiliko yoyote kiuchumi, kama mashine ya maji ya kijiji cha Sinya yenye zaidi mwaka bila kutumika.

Baraza hili la mila waliona kuwa, huenda uwekezaji una nia njema ya kuboresha uchumi lakini hawakuridhika na vyombo vya uwakilishi na utoaji maamuzi. Walisema kuwa baada ya kutafakari kwa undani imeonekana kuwa manufaa ya uwekezaji umekusudiwa kuwanufaisha viongozi na wawakilishi wengine. Mfano mojawapo ni chombo cha kusimamia WMA kwenye kijiji kimoja, walisema kuwa chombo hicho ni cha kifamilia. Kama kweli uwekezaji huo ni wa manufaa kwa wanavijiji imekuwaje kikawa cha kifamilia? Hali kadhalika manufaa ya uwindaji na utalii wa picha, imesemekana kuwa makusudio ya wawekezaji hao ni kujinuifaisha wenyewe na si kuwanufaishawanavijiji. Sababu nyingi zilitolewa kueleza mapungufu katika uwindaji na utalii wa picha.

Changamoto kwa wanawarsha ni kwamba serikali imekubali kuimarisha uwekezaji na imekubaliana na sera za uwekezaji. Hivyo basi ni nafasi ya wafugaji kujua watashiriki na kukabiliana vipi na uwekezaji na madhara yatokanayo na uwekezaji hasa wa ardhi. Wanawarsha wameona na kukubaliana kuwa jamii ya wafugaji hawana habari na mabadiliko hayo ya kiuchumi duniani, hivyo hubakia kulalamika bila kutambua misukumo ya ardhi yanasababishwa na nini. Kutoshirikishwa katika maamuzi imeleta mitazamo ngeni katika suala zima la maendeleo yao wenyewe.

Baraza hili limeona kuwa kuna haja ya kuelimisha jamii kupitia Bazara la mila, serikali za vijiji na mikutano mikuu ya vijiji ili kujenga hamasa ya pamoja ndani ya jamii. Walisema kuwa jamii inamitazamo tofauti na maendeleo ya sasa, kwani kama tutaendelea kushikilia ufugaji ni muhimu kujua uhakika wa ardhi na maamuzi ya watu juu ya uwekezaji. Na muhimu zaidi ni manufaa yatokayo na aina yoyote ya uwekezaji kwenye ardhi ya vijiji. Walisisitiza kuwa elimu si kusoma tu na kuandika bali ni ufahamu juu ya maisha na jinsi gani ya kutatua matatizo ya maisha.

Mada ya Tano **Uchambuzi wa jamii.**

Uwakilishi.

Mada hii itajadiliwa kwa kirefu na ilionekana kuwa pamoja na mapungufu mengi ya jamii ya wafugaji vyombo vya uwakilishi katika ngazi mbalimbali hazina uhusiano wa pamoja, kila moja inafanya kazi pasipo kujali nafasi ya nyingine. Vyombo vya uwakilishi vilivyojadiliwa ni pamoja na Baraza la mila, serikali za vijiji, kamati za maendeleo vya kata, Baraza la madiwani, mashirika yasiyo ya kiserikali hivyo ni vyombo muhimu katika maamuzi na uwakilishi.

Baada ya kutafakari kwa undani zaidi mambo yafuatayo yalijitokeza:-

- Ushirikishwaji duni wa maamuzi yahusianayo na maisha ya jamii,
- Kutokwepo na mchakato sahihi wa kujadili mtazamo wa maendeleo na jamii.
- Chombo la mila cha uongozi kunyima kufanya kazi na balada yake vyombo mbadala kuchukua nafasi katika mfumo wa maisha unaotawaliwa na mila

Dhana ya uwakilishi na ushirikishwaji hasa ya mipango na maamuzi yamekuwa yakihubiriwa pasipo kutekelezwa kupitia vyombo shirikishi, ndiyo maana jamii ya wafugaji wamebakia nyuma kimaendeleo. Baada ya mjadala mrefu, ilionekana kuwa vyombo vya uwakilishi vina nafasi ya kuimarisha ushirikishwaji na kuleta mabadiliko ya kimaendeleo, endapo umma na vyombo venyewe vitatambua wajibu wao.

Washiriki pia walitambua pia kuwa mfumo wa uongozi wa mila (Laigwanak) umeadhiriwa na mabadiliko makubwa ya kiuchumi, kijamii na kisiasa, na chombo hicho muhimu kubakia pasipo kutekeleza wajibu wake.

Viongozi wa mila (Ilaigwanack lolosho)

Viongozi wa mila (Ilaigwanack) huchaguliwa na jamii kufuatilia masuala mbalimbali yahusianayo na mila. Katika jitihada za kuleta maendeleo na kuondokana na umaskini viongozi hao wamekuwa wakitumiwa na serikali katika masuala ya kuhamasisha jamii katika michango ya maendeleo.

Viongozi hao wa mila walieleza kuwa maamuzi mbalimbali yalionyeti hasa yahusianayo na ardhi na maliasili hawahusishwe na kutohusika kwao imesababisha mgawanyiko wa jamii hasa katika maamuzi.

Baadhi ya llaigwanack wamekumbwa na wimbi la mabadiliko ya kisiasa na kujikuta wakiwa na mamlaka mengine kama wenyeviti wa vijiji, vitongoji, ili kupata nafasi ya kujihusisha na masuala ya jamii. Mtafaruku wa viongozi wa mila imezorotesha mshikamano wa baraza la mila na uongozi wa mila. Imeonekana pia kuwa kwa mifumo ya uongozi hasa wa mkondo wa sheria na serikali haileti mwenendo sahihi ya mshikamano wa jamii itakayojadili masuala nyeti kama kupotea kwa ardhi na njozi ya baadaye ya jamii, kwa sababu wawakilishi huongozwa na mitazmo tofauti na maamuzi ya jamii husika.

Vyombo vya uwakilishi katika ngazi zote vimeonekana kutokuwa na njozi na uwezo wa uwakilishi kutokana ufahamu mdogo wa nini kifanyike, lini na kwa nani, vyombo hivi havitambuwi wanawajibike kwa nani na pia kukwepa uwajibikaji wao. Hata hivyo hawajisikii kama wanawajibika kwa jamii na hivyo kusaidia jamii kujikomboa kiuchumi na kisiasa.

Kwa hali hii ya kutokuwepo na uwajibikaji, uwazi katika njozi, jamii kwa ujumla wanajikuta kukosa uelekeo wa kujiletea maendeleo na maendeleo ya mfumo upi. Kukosa uelekeo wa kujiletea maendeleo endelevu jamii, viongozi hao wameona haja ya kujenga umoja wao wa kuleta mtazamo mpya wa maisha. Washiriki walitambua nafasi ya mashirika binafsi, ambao yamaekuwa mstari wa mbele kujaribu kuelekeza na kuelimisha jamii juu ya maendeleo endelevu yakiwa kama chombo binafsi cha kuwakilisha jamii, ili imeonekana kuwa mashirika hayana nguvu kisiasa, hivyo kwa wakati mwingine inakuwa vigumu kwao kuleta changamoto. Na hata hivyo mashirika huwa na matakwa yao binafsi ambayo haendani na jinsi jamii inavyotaka kuwa. Hivyo kuna haja ya kuwa na chombo cha kusaidia serikali kuwaleta pamoja jamii na kujenga mtazamo halali wa kufikia njozi endelevu.

Viongozi hao wa mila wamejadili kuwa, kuna haja ya jamii ya wafugaji kuungana na kujenga '*Olkiama*' baraza ambalo litashawishi matakwa ya jamii katika ngazi ya sera na sheria ya Nchi hasa suala la ardhi, ufugaji na manufaa yatokanayo na maliasili. Walitoa mfano wa '*Olkiama*' wakati wa utawala wa kikoloni. Walisema *Olkiama* ilishawishi serikali ya kikoloni kutoa kipaumbele katika suala la huduma ya mifugo kama maji, majosho na tiba ya milipuko ya magonjwa ya mifugo na masoko. Waliendelea kusema kuwa vyombo vilivyochukua nafasi ya '*Olkiama*' hawazingatii ufugaji wa mifugo, na hii imeleta hasara kubwa kwa maendeleo ya mifugo. Kwa mfano maneneo mengi yenye malisho mazuri wakati wa kiangazi hakuna maji. Pia ili dhana kuanzisha Range za mifugo imebadilishwa na kudhoofishwa na imeatifishwa na kubakia kwa serikali au watu binafsi na

hayo yalikuwa maeneo ya wafugaji ya kulishia mifugo yao. Baadhi ya range ni kama shamba la west kili la serikali, manyara na mengine mengi.

Baada ya kutafakari masuala nyeti juu ya nafasi ya uwakilishi na maendeleo endelevu, viongozi hao wa mila walihitaji kujua mahitaji ya jamii hasa kimaendeleo kiuchumi na kisiasa. Ili kujua mahitaji ya lazima na nini kifanyike waliweka vipaumbele matatizo mbalimbali.

Matatizo kwa vipaumbele.

Elimu: Elimu ilijadiliwa kuwa ni tatizo kubwa sana kwa jamii. Elimu ilitazamwa kwa njia kuu mbili. Elimu ya kujua kusoma na kuandika kwa watoto wa kifugaji. Viongozi hao wamejadili kuwa elimu kwa watoto katika ngazi zote ni duni sana. Walisema pamoja na kuwaweka watoto shuleni bado kuna upungufu mkubwa wa ubora wa elimu ndani ya wilaya. Watoto wachache sana hufanikiwa kwenda sekondari baada ya kushindwa kufauli mtihani wa darasa la saba. Hivyo hili ni tatizo kubwa sana ndani ya wilaya ya Longido.

Kipengele kingine cha Elimu ni kwa viongozi wa jadi na jamii kwa ujumla; kuwa jamii na viongozi wao hawana ufahamu wa masuala yanayohusu maisha yao. Walieleza kuwa hawajui sera na sheria zinazotoa miongozo mbalimbali katika nchi. Kwa mfano mabadiliko ya sheria ya Ardhi, MKUKUTA, MKURABITA, sera na sheria ya wanyamapori na mabadiliko ya dunia kuhusu suala zima la maendeleo kuichumi na kisiasa. Baadhi yao walisema hatujawai kuona katiba ya nchi na hata kusoma. Waliendelea kusema kuwa bila kupata ufahamu wa nini kinachoendelea katika serikali yao, hawataweza kuleta maendeleo sahihi kwa maisha yao na watoto wao baadaye.

Ardhi: Ardhi ilionekana kama ni tatizo nyeti pia, walisema kuwa ardhi sasa imekumbwa na misukumo ya ndani na nje. Misukumo hii inaatarisha uwepo wa ardhi na hatimaye maisha ya jamii ya wafugaji. Walieleza kuwa suala la matumizi ya ardhi sasa imezidiwa kwani kuna milipuko tofauti na ufugaji juu katika ardhi ya vijiji. Milipuko hizo ni kama uwindaji wa wanyamapori iliyowekwa na serikali mikononi mwa wawindaji wenyewe, utalii picha ambao wanadai maeneo ya kupiga kampi za kitalii, maeneo ya hifadhi katika ardhi za vijiji kama Hifadhi za Jamii (WMAs) na matumizi mengine ya maliasili kama uchomaji mkaa, n.k.

Wanyamapori na Maisha ya watu:-

Viongozi hao wanasema kuwa tatizo la wanyamapori Longido imekuwa kubwa mno. Wanyamapori hasa tembo wanaendeleo kuwadhuru watu wengi pasipo malipo juu maisha ya watu yao. Walieleza matukio matatu ya mwezi moja katika baadhi ya vijiji vya west kili. Walisema kuwa ni jukumu la viongozi wa mila, Mbunge na DC kuona ni jinsi gani ya itakabiliana na madhara

yatokayo na wanyamapori, la sivyo maisha ya jamii itakuwa hatarini kwa siku za usoni. Hili linaweza kujenga uadui wa jamii na wanyamapori, kinyume na vile ilivyokuwa awali. Suala hili la wanyamapori na maisha ya watu, ilionekana na viongozi wa mila kuwa hakuna mapato yoyote yatokayo na wanyamapori yanayosaidia kuondoa umaskini katika vijiji vyao. Kwa hali hiyo basi waliona kuwa kuna haja ya viongozi wa mila na serikali kujadili ni jinsi gani jamii inaweza kunufaika na mapato yatokayo na wanyamapori na kulipiwa fidia mara wanyamapori wakisababisha madhara kwa jamii.

Mapendekezo ya warsha:-

Viongozi wa mila waliomba mashirika wawezeshaji kuwajengea uwezo juu ya mambo yafuatayo:-

- Kuwezesha umoja na ushirikinao wa viongozi wa mila ili kuimarisha baraza la mila la wilaya na hatimaye '*Olkiama*' kwa ajili ya jamii ya wafugaji mkoa wa Arusha na Manyara.
- Kuelimisha baraza la mila juu ya sera na sharia mbalimbali hasa ya ardhi, wanyamapori na sera za kukuza uchumi kama MKUKUTA na MKURABITA.
- Kusaidia katika kuimarisha utambulisho rasmi ya mabaza la mila kwa serikali kupitia katiba ya Laigwanack.

Hitimisho juu ya warsha.

Warsha hii imewawezesha viongozi wa jadi na wazee wengine mashuhuru kupata fursa ya kujadili maisha yao na watoto wao kwa sasa na baadaye. Majadiliano haya baina ya viongozi wa mila na wazee mashuhuru '*Ingopirr*' pamoja na wawezeshaji ni mwanzo mzuri wa kuleta uelekeo wa jinsi maisha ya wafugaji wilaya ya Longido itakavyokuwa. Mijadala kuhusu matatizo hasa ya ardhi na maliasili, uongozi na uwakilishi wa jamii ndiyo msingi thabiti ya kufikia maamuzi ya msingi katika kujenga njozi na kuleta mabadiliko ya haraka ya maendeleo ya jamii hii. Kujenga mtandao wa jamii ya uongozi ngazi ya chini na hatimaye ngazi za juu za wilaya na Taifa itakuwa changamoto ya kufikia demokrasia katika maendeleo. Warsha hii ilitambua kuwa maendeleo halisi ni ya watu kujiletea wenyewe katika kujadili na kufikia maamuzi ya kutafakari dira ya maisha.

RATIBA YA WARSHA

MUDA	NINI	NANI
2.30 – 3.00	Kutambulishana na Ufunguzi	Wote
3.00 - 4.30	Masomo	Wote
4.30 - 5.00	Chai	Wote
5.00 - 7.00	Masomo	Wote
7.00 - 8.00	Chakula	Wote
8.00 - 9.00	Masomo	Wote
9.00 - 10.30	Masomo	Wote
10.30 -	Kufunga	Wote